

# Bima Mpya ya Watu Wazima

*Inaanza Januari 1 2019, Watu wazima wengi waishio Virginia wanaweza kupata bima ya afya bora, nafuu na bure!*

## 1. Bima Mpya ya Afya kwa Watu Wazima ni Nini?

Kanuni za Medicaid zimebadilika. Hii ina maana kuwa kama uliomba Medicaid siku za nyuma na ukanyimwa, sasa unaweza kupata. Kuanzia Novemba 1, 2018, watu wengi wanaweza kuomba na kupata sifa ya kuwa na bima ya afya kupitia Medicaid. Kunufaika itaanza Januari 1, 2019.

Watu wanaofanya biashara, ujezi, kulea watoto, kutengeneza mandhari, huduma za chakula na kazi zingine nyingi ambazo hazitoi bima ya afya, kwa sasa wanaweza kupata bima.

Bima mpya ya afya kwa watu wazima ni ya manufaa makubwa kwa familia zenye kipato kidogo ambazo zisingeweza kupata huduma za afya.

## 2. Bima hii inatoa nini?

Bima mpya ya afya kwa watu wazima hutoa:

- Huduma za daktari, hospitali na ya dharura
- Madawa aliyoandikiwa mgonjwa
- Huduma za maabara na mionzi ya X-ray
- Huduma za mtoto na mjamzito
- Huduma na msaada wa muda mrefu
- Huduma za afya nyumbani
- Huduma za afya ya tabia ikiwemo uraibu na huduma za kupata nafuu au kupona ugonjwa
- Huduma za kupunguza athari za madawa ikiwemo za mwili, kikazi na tiba za kurekebisha uwezo wa kuongea.
- Usafiri wa kupelekwa palipo na huduma za Medicaid pale ambapo hakuna mbadala.
- Huduma za uzazi wa mpango
- Vifaa tiba na vitendea kazi vingine.
- Huduma za ustawi na za kinga na uthibiti wa magonjwa sugu
- Na mengine mengi!

## 3. Nani anastahili?

Watu wazima watastahili bima mpya kama:

- Wanaishi Virginia
- Wana umri wa miaka 19 – 64
- Hawana sifa za kupata Medicare
- Wanafikia hitaji la kipato, ambacho hutofautiana kwa ukubwa wa familia.

## Kikomo cha Kipato kwa Bima ya Watu Wazima (Ghafi)\*

| Ukubwa wa familia | Kwa Mwezi | Kwa Mwaka |
|-------------------|-----------|-----------|
| 1                 | \$1,482   | \$17,775  |
| 2                 | \$2,004   | \$24,040  |
| 3                 | \$2,526   | \$30,305  |
| 4                 | \$3,048   | \$36,570  |
| 5                 | \$3,570   | \$42,836  |
| 6                 | \$4,092   | \$49,101  |

\*Kuanzia Januari 13, 2021. Kikomo cha kipato hubadilishwa kila mwaka.

## 4. Ninaombaje?

Unaweza kuomba bima ya afya kwa kutumia njia yoyote kati ya hizi zifuatazo:

- Pigia simu Kituo cha Bima kwa 1-855-242-8282. Wakalimani wanapatikana. Wawakilishi wetu watakuunganisha na mtu anayejua lugha yako.
- Jaza fomu kwenye mtandao wa Msaada wa Kawaida (Common Help): [www.commonhelp.virginia.gov](http://www.commonhelp.virginia.gov)
- Jaza maombi mtandaoni kwenye The Health Insurance Marketplace: [www.healthcare.gov](http://www.healthcare.gov)
- Tuma au ulete fomu ya maombi katika Idara ya Huduma za Jamii iliyopo karibu yako.

Kupata orodha ya nyaraka ambazo utazihitaji wakati wa kufanya maombi, tembelea, [www.coverva.org](http://www.coverva.org) na ubonyeze sehemu ya ukurasa wa 'Apply'.

